

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



TAARIFA KWA UMMA

**KUSITISHA MICHEZO YA UMISETA, UMITASHUMTA NA MAELEKEZO KUHUSU
MAHAFALI YA KIDATO CHA SITA**

Kama tunavyofahamu kuwa ugonjwa wa Corona ni hatari na unaua kwa haraka lakini mpaka sasa katika Nchi yetu haina mgonjwa wa maambukizi ya virusi hivi kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Pamoja na taarifa hiyo bado tumetakiwa kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya CORONA. Nikiwa kama Waziri mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na ambaye nasimamia utoaji wa Elimu kuanzia ngazi ya msingi mpaka sekondari Nchini naelekeza kuwa kwa mwaka huu 2020 mashindano ya michezo ya UMISETA na UMITASHUMTA yaliyokuwa yafanyike hivi karibuni yamehairishwa mpaka hapo mtakapotangaziwa.

Hivyo wanafunzi wote wanaohusika na michezo hii kuanzia ngazi ya msingi mpaka sekondari wanatakiwa kubaki kwenye shule zao na kuendelea na masomo yao kama kawaida.

Aidha, kwa Kidato cha sita ambao wengi wao katika shule zao wanategemea kufanya sherehe za mahafali (Graduation) katika siku za usoni. Naelekeza kuwa sherehe hizo zisihusishe wageni kutoka nje ya shule kama kuna ulazima wa kufanya mahafali, na yafanyike kwa kuwahusisha wanafunzi pamoja na jamii ya shule tu na sio wageni kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Hii ni kwa nia njema ya kuendelea na mikakati na maelekezo ya Wizara ya Afya na msisistizo mkubwa uliotolewa na **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** juu ya kuepuka misongamano isiyokuwa na lazima katika kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa Corona.

Imetolewa na:

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Selemani S. Jafo'.

Selemani S. Jafo (Mb)
Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI
15/03/2020